Yehova Au Farao, Nani Zaidi?

Na

Ellis P Forsman

(Jehovah Or Pharaoh, Which?)

Yehova Au Farao, Nani Zaidi?

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 12, 20

Yehova Au Farao, Nani Zaidi?

Kut. 5:1-23

Musa na Haruni walikuja mbele ya Farao kumuomba awaruhusu Waisrfaeli waondoke na kuabudu jangwani.

Kut. 5:1, "*Hata baadaye Musa na Haruni wakaenda wakamwambia Farao, wakasema BWANA Mungu wa Israeli asema hivi wape watu wangu ruhusa waende ili kunifanyia sikukuu jangwani.*"

Walihitaji kuondoka kwa jina la Bwana.

Lakini Farao akajibu hitaji lao kwa kumuasi Mungu. Kut. 5:2, "*Farao akasema BWANA ni nani hata niisikilize saauti yake, na kuwapa Israeli ruhusa waende zao? Mimi simjui BWANA na wala sitawapa Israeli ruhusa waende zao.*"

Mara ya kwanza, Farao alikataa katakata – "*sitawapa Israeli ruhusa waende zao.*"

Lakini Mungu alituma pigo baada ya pigo dhidi ya Farao na watu wake (mto kugeuka damu; pigo la vyura, chawa, na nzi); alafu Farao akaanza kufanya mapendekezo.

Ebu tuangalie uerevu nne na mapendekezo ya muafaka wa Farao.

Pendekezo la kwanza

Kut. 8:25, "*Farao akawaita Musa na Haruni akawaambia endeni mkamtolee Mungu wenu dhabihu ndani ya nchi hii.*"

Lakini mpango huu haukufanya kazi. Kut. 8:26, "*Musa akasema haitupasi kufanya hivyo; kwa kuwa tutamchinjia sadaka BWANA Mungu wetu na haayo machukizo ya Wamisri; Je! Tutachinja sadaka ya hayo machukizo ya Wamisri mbele ya macho yao, wasitupige kwa mawe?*

Ingekuwa ni kosa kwa Mungu kama wangechinja dhabihu ya Wamisri, na pia ingekuwa ni kosa kwa Wamisri kama wangemtolea Mungu dhabihu yao wenyewe.

Vilevile, wasingeweza kufanya dhabihu katika nchi bila kibali toka kwa Mungu au kwa wakuu wao.

Mpango huu ungewafanya wawe katika wakati mgumu na Wamisri wasiotahiriwa, na hivyo kumuweka Yehova katika kiwango sawa na miungu wa Misri.

Katika shauri hili, Mmisri angeweza kusema, "Sioni tofauti kati yetu; mnaibaada yenu nasi tunayo yetu; lakini zote ni ibada."

Wapo wale wanaotumia na kukubali vitu vigeni katika ibada wale wanaotuambia, "Hakika hakuna tofauti kati yetu."

Ni tofauti ambayo inafanana kati ya kweli na upotoshaji, au wemaa na ubaya. Yohana 8:32, "*Mtaifahamu kweli nayo kweli itawaweka huru.*"

Hakuna mkato ambao haujakamilikaa utakaompendezaa Mungu. 2 Kor. 6:14-17, "*Msifungiwe nira paamoja na wasioamini, kwa jinsi ilivyo sawasawa; kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi? Tena pana shirika gani kati ya nuru na giza? Tena pana ulinganifu gani kati ya Kristo na Beliali? Au yeye aaminiye ana sehemu gani pmoja na yeye asiyeamini? Tena pana mapatano gani kati ya hekalu la Mungu na sanamu? Kwa maana sisi tu hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu alivyosema ya kwamba nitakaa ndani yao na kati yao nitatembea, nami nitakuwa Mungu wao nao watakuwa watu wangu. Kwaiyo tokeni kati yao mkatengwe nao, asema Bwana, msiguse kitu kilicho kichafu, nami nitawakaribisha.*"

Hakukuwa na sehemu ya kukutania kwa watu wa Yehova kule Misri. Hakukuwa na hekalu, wala madhabahu.

Wokovu ambao ungewaacha Misri usingeweza kuwa wokovu wa Mungu.

Hivyo basi, Musa akaongea na Farao kwa upole kwamba yeye na ndugu zake wangependa kufanya mapenzi ya Yehova. Kut. 8:27, "*La tutakwenda safari ya siku tatu jangwani, tumchinjie dhabihu BWANA, Mungu wetu kama atakavyotuagiza.*"

Ndivyo, inavyotakiwa kuwa kwa Wakristo pia – anapaswa ajisulubishe mwenyewe katika dunia.

- Gal. 2:20, "*Nimesulibiwa pamoja na Kristo lakini ni hai; wala si mimi tena bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu.*"
- Gal. 6:14, "*Lakini mimi hasha nisione fahari juu ya kitu chochote ila msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambao kwa huo ulimwengu umesulibishwa kwangu, na mimi kwa ulimwengu.*"

Hivyo, msalaba wa Kristo siyo tu umeondoa dhambi ya Mkristo, bali pia imeondoa kabisa mahusiano yake na ulimwengu.

- Rom. 6: 1-4, "*Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi? Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima.*"
- Rom. 6:6-7, "*Mkijua neno hili ya kuwa utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye ili mwili wa dhambi ubatilike tusitumikie dhambi tena.*"
- Rom. 6:12, "*Basi dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tamaa zake.*"

- Rom. 12:2, "*Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema ya kumpendeza, na ukamilifu.*"

Mkristo anapaswa kutembea katika roho.

- Gal. 5:16, "*Basi nasema enendeni kwa Roho wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili.*"
- Zaburi 1:1-2, "*Heri mtu yule asiyekwendaa katika shauri la wasio haki; wala hakusimama katika njia ya wakosaji; wala hakuketi katika barazani pa wenye mizaha. Bali sheria ya BWANA ndiyo impendezayo, na sheria yake huitafakari mchana na usiku.*"

Pendekezo la pili

Kut. 8:28, "*Farao akasema mimi nitawapa ruhusa mwende ili mmchinjie dhabihu BWANA Mungu wenu jangwani; lakini hamtakwenda mbali sana; haya niombeeni.*"

Pendekezo hili lilifanana zaidi na la kwanza.

Wakati pendekezo la kwanza lilipokataliwa, basi farao akawaruhusu waende jangwani, lakini "*siyo mbali sana*."

Labdaa Farao aalisikiaa kitu nkuhusu wao kwenda Kanani na akahisi kwamba mara watakapoondoka Misri, hawatarudi kamwe. Hivyo hakupenda waondoke mbele ya macho yake.

Kama hasingeweza kuwaweka Misri, angeweza kuwaweka karibu nayo, ili kwamba aendelee kuaminiwa juu yao.

Kwa njia hii wangeweza kurudishwa tena, na hapo hushuhuda wao ungekuwa imara zaidi kuliko wasingeondoka Misri kamwe.

Mara zote kunakuwa na uharibifu kwa sababu ya Kristo kwa watu wanaonekana wanao acha ulimwengu, alafu badae wanairudia tena, kuliko ambavyo wangeendelea kubaki ndani yake.

2 Pet. 2:20-21, "*Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho inakuwa mbaya kuliko ile yaa kwanza. Maana ingekuwa heri kwao kama wasingaliijua njia ya haki kuliko kuijua kisha kuiacha ile amri takatifu waliopewa.*"

Hivyo basi, kama watu hawaendi "*mbali sana*" ni afadhali wasingeenda kamwe.

Pendekezo la tatu baada ya pigo la wanya kufa

Kut. 10:8-11, "*Ndipo Farao akawaita Musa na Haruni na kuwaambia mwombeni BWANA ili awaondoe vyura hawa kwangu na kwa watu wangu nami nitawapa watu ruhusa waende zao ili wamtolee BWANA dhabihu. Musa akamwambia Farao, haya ujitukuze juu yangu katika jambo hili; sema ni lini unapotaka nikuombee wewe na watumishi wako, na watu wako ili hao vyura waangamizwe watoke kwako wewe naa nyumba zako, wakae ndani yam to tu. Akamwambia,*

kesho, akasema, na yawe kama maneno yako; ili upate kujua ya kwamba hapana mwingine mfano wa BWANA Mungu wetu. Hao vyura wataondoka kutoka kwako wewe na nyumba zako, na watumishi wako na watu wako; watasalia mtoni tu."

Farao alijua kwamba kadiri anavyowazuia wana wa Israeli Misri, wangeweza kubaki utumwani kwa ajili yake.

Vivyo hivyo, Shetani pia anajua kwamba kadiri watoto wetu hawabaki kuwa Wakristo, wanabaki utumwani kwa ajili yake.

Tunaposisitiza kwamba watu wa Mungu ni "*watu wateule*" (1 Pet. 2:9), neno linasema, "*Lakini hiyo haimanishi kwamba watoto wako wanapaswa kuwa hivyo.*"

- Wazazi wengi wamevutiwa na filosofia hii mbayaa, maana wamekwenda kumwabudu Mungu, na kuwaacha watoto wao Misri.
- Kuna juhudi chache za kuweka thamani ya Ukristo kwa watoto wao na kuwafundisha maneno toka kwa Mungu.
- Wazo ni kuwaacha wapende mbengu mbaya kwanza, alafu waache wafikirie katika akili zao kama wanataka kumtumikia Mungu, au la.
- Kama mtoto anakua pasipokumjua Kristo, anawezaje kuanza kumfuata kwa umakini?

Wazazi jangwani; na wana wa Israeli Misri – wazo bayaa. Huku kusingeweza kuwa kuondolewa kuliko kamilika.

Kama Waisraeli walibaki Misri, wazazi wasingesemwa wameondoka, maana watoto wao pia walikuwa sehemu yao.

Zaidi ambacho kingesemwa kuhusu swala hili ni kwwambaa walikuwa wanamtumikia Yehova kwa sehemu na kwa sehemu Farao.

Lakini Yehova hakuwa na sehemu na Farao; alitamani vyote au hakutamani.

Mat. 6:33, "*Basi utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.*"

Huu ndio ukweli ambao wazazi wanatakiwa kujifunza – kwamba ni jukumu lao kuwalea watoto wao katika njia inayompendeza Bwana.

- Mhu. 12:1, "*Mkumbuke muumba wako siku za ujana wako, kabla hazijaja ssiku zilizo mbaya, wala haijakaribia miaka utakaposema, mimi sina furaha katika hiyo.*"
- Kumb. 11:18-21, "*Kwa hiyo yawekeni maneno yangu mioyoni mwenu na rohoni mwenu; yafungeni yawe dalili juu ya mikono yenu, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yenu. Tena yaandike juu ya miimo ya nyumba yako, na juu ya malango yako; ili siku zenu zifanywe nyingi, na za vijana vyenu nao, juu ya nchi BWANA aliyowaapia baba zenu kuwa atawapa, kama zilivyo siku za mbingu juu ya nchi.*"
- Mit. 22:6, "*Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee.*"

Hatupaswi kuridhika na sehemu yoyote ya dini kwa watoto wetu kuliko kile tufanyalo na kufurahia.

Pendekezo la nne – acha makundi yenu yakae

Ilitokea baada ya pigo la jipu, pigo la mvua yam awe na moto, pigo la nzige walioharibu mazao yao, na giza kubwa juu ya nchi kwa siku tatu.

Kut. 10:24, "*Farao akamwita Musa na kumwambia haya nendeni mkamtumikie BWANA; kondoo zenu na ng'ombe zenu tu na waachwe; watoto wenu nao na waende pamoja nanyi.*"

Ni mwendelezo ulioje! Farao alipinga kila nukta ya njia ya Waisraeli kutoka Misri!

- Kwanza aliwaza kuwaacha wakae katika nchi.
- Alafu kuwaweka karibu na nchi.
- Alafu kuweka sehemu yao katika nchi – watoto wao.
- Na sasa, mwishowe, aliposhindwa kufaulu katika mapendekezo yote matatu, aliamua kuwaruhusu waondoke bila vitu vyao.

"Nendeni jangwani kama mnaweza, lakini acha biashara zenu Misri."

Shetani anapenda kikamilifu kwamba tuwe wacha Mungu na wenye maombi kama tunavyotaka iwe jumapili, akijua kwamba tunasahau yote juma tatu.

Anapenda tujitoe katika dini kama tutageuza dini zetu katika nyumba za kanisa.

Lakin dini isiyoingi na kuchanganya biashara na uhusiano wa kibiashara, siyo dini ya Yesu Kristo.

2 Kor. 10:5, "*Tukiangusha mawazo na kila kitu kilichoinuka, kijiinuacho juu ya elimu ya Mungu; na tukiteka nyara kila fikira ipate kumtii Kristo;*"

Jibu la Musa. Kuto. 10:26, "*Makundi yetu pia watakwenda pamoja nasi; hauta salia nyuma hata ukwato mmoja; kwa maana inampasa kutwaa katika hao tupate kumtumikia BWANA Mungu wetu; nasi hatujui hata tutakapofika huko ni kitu gani ambacho kwa hicho inatupasa kumtumikia BWANA.*"

Misri siyo sehemu ya wakombolewa wa Mungu.

Hivyo basi, tusiache chochote nyuma – hata tunavyo vimiliki, au sisi wenyewe, au wapendwa wetu, au yale yanayoturidhisha; ili kwamba kusiwe na jaribu la kuangalia nyuma.

Yesu alisema kwambaa sisi ambao ni wanafunzi wake hatupaswi kuangalia nyuma.

- Luka 9:62, "*Yesu akamwambia mtu aliyetia mkono wake kulima kisha akaangalia nyuma, hafai kwa ufalme wa Mungu.*"

- Luka 17:32, "*mkumbukeni mkewe Lutu.*"

Yeye aingiaye katika huduma ya Kristo ni lazima aifanye kwa moyo wake wote. Lazima aachane na ulimwengu, maana yeye ajaye lakini bado anaupenda ulimwengu, akiwa anaangalia kwa huzuni kwamba wameacha mambo mazuri yaaliyoko duniani na heshima, ambaye hajaziacha, hakika hawezi kuwa Mkristo.

Hitimisho

Yesu anafaa. 1 Kor. 6:19-20, "*Au hanjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi mtukuzeni Mungu katika miili yenu.*"

Hatupaswi kuwa na kuridhika katika moyo wa Mkristo ambaye Kristo hasingependa awe sehemu yake.

Hakika hadithi hii ni mfano wa kupenda katika umri wetu, ikifunua umuhimu wa utii na kutengwa kabisa na dunia.

- Wito wa Mungu ni kutengwa, lakini ulimwengu unatusihi tuendelee kubaki katika nchi na kuwa karibu.
- Mapenzi ya Mungu ni kwamba tuwe na umbali katika nchi ya jirani yetu.
- Alafu ulimwengu utasema kwamba tukisisitiza kuwa wateule, siyo muhimu kuwaambia watoto wetu kuwa hivyo pia.

Wakati ulimwengu unasisitiza kwamba tuache tunavyovimiliki nyuma, tunapaswa kukumbuka kwamba ni muhimu kwamba tufanye shughuli zetu kwa amani na roho wa kweli ya Mkristo. Na kwamba miliki zetu, pia, zitumike katika utukufu wa Mungu, kwa hakika, "*Hautasalia nyuma hata ukwato mmoja.*"